# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

## HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

**MEI, 2025**

**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

70 Barabara ya Chukwani,Buyu
70490 Mjini Magharibi,
S. L. P 902 Chukwani,
Zanzibar, Tanzania

Simu: +255 24 224 2000
Nukushi: +255 24 224 2000
info@zanzibarassembly.go.tz
www.zanzibarassembly.go.tz

## HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

**Mheshimiwa Spika,** Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, alietupa fursa ya kukutana tena katika muendelezo wa kikao chetu, tukiwa wenye afya njema. Tunamuomba Allah Mtukufu atupe nguvu na marifa za kutimiza majukumu yetu ya kuwatumikia wananchi kwa salama, amani na utulivu hasa katika kipindi hichi cha matayarisho ya uchaguzi mkuu wa 2025.

**Mheshimiwa Spika,** shukurani za pekee zikufike wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii adhimu ya kusimama mbele ya Baraza hili kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu ***Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mwaka wa fedha 2025/2026.***

**Mheshimiwa Spika:** kwa dhati kabisa napenda kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa jitihada zake za kusisitiza umuhimu wa kudumisha amani na utulivu kila anapokutana na viongozi mbali mbali wa Serikali, vyama vya siasa, viongozi wa kidini na wananchi katika maeneo mbali mbali. Sambamba na kuyakemea vikali masuala yenye kurudisha nyuma nguvu kazi za taifa ikiwemo masuala ya UKIMWI na dawa za kulevya. Tunamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu azidi kumpa weledi na uimara wa kusimama tena kwa awamu ya pili ya

kuwatumikia wananchi ili kukamilisha yale yote aliyokusudia kwa mustakbali wa wananchi wa Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,** pongezi Mahsusi zimfikie Makamu wa Kwanza wa Rais, Mheshimiwa Othman Masoud Othman kwa kuhakikisha anatimiza wajibu wake wa kumsaidia na kumshauri Mheshiwa Rais ipasavyo katika Nyanja za kiuchumi, kijamii, kisiasa na masuala ya mtambuka ambayo ndio kiini cha utendaji wa Ofisi yake. Pamoja na mashirikiano makubwa anayoyapata kutoka kwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Mheshimiwa Harusi Said Suleiman kwa kufanya kazi bega kwa bega katika kipindi chote cha uhai wa kamati hii akisaidiana na watendaji wa Ofisi yake wakiongozwa na Katibu Mkuu Bi Maryam Juma Abdalla Sadalla. Aidha, kipekee tuwashukuru watendaji wa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kwa mashirikiano yao walioyaonyesha wakati wa kupitia rasimu ya Makadirio ya Bajeti ya Ofisi hii kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

**Mheshimiwa Spika:** shukurani za pekee ziwaendee Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati yangu kwa jinsi tunavyoshirikiana katika kutekeleza majukumu ya Kamati hii na kuhakikisha kuwa ufatiliaji wa matumizi ya fedha za bajeti zinaendana na thamani halisi ya fedha inapatikana katika kazi za Wizara hii na kila Taasisi zake.

**Mheshimiwa Spika:** Kwa heshima na taadhima, naomba sasa kuwatambua Wajumbe hao kwa majina kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| *1.* | Mhe. Machano Othman Said | Mwenyekiti |
| *2.* | Mhe. Maryam Thani Juma | Makamu Mwenyekiti |
| *3.* | Mhe. Zaina Abdalla Salum | Mjumbe |
| *4.* | Mhe. Mussa Foum Mussa | Mjumbe |

| | | |
|---|---|---|
| *5.* | Mhe. Haji Shaaban Waziri | Mjumbe |
| *6.* | Mhe. Abdalla Abass Wadi | Mjumbe |
| *7.* | Mhe. Suleiman Haroub Suleiman | Mjumbe |
| *8.* | Mhe. Jamal Kassim Ali | Mjumbe |
| *9.* | Ndg. Ali Alawy Ali | Katibu |
| *10.* | Ndg. Mwanaisha Mohammed Kheir | Katibu |
| *11.* | Ndg. Shawana Mohammed Haji | Katibu na |
| *12.* | Ndg. Amina Abeid Hemed | Mkalimani |

**Mheshimiwa Spika:** naomba tukumbuke kuwa, majukumu ya msingi ya Kamati ni kuchambua mapendekezo ya Serikali kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Fedha ya Wizara husika na mwaka husika. katika kutekeleza jukumu hilo, Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ilipitia, kujadili na hatimae kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

**Mheshimiwa Spika:** Kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Kamati yangu naomba niwasilishe mbele ya Baraza lako Tukufu maoni kuhusiana na mafungu ya bajeti ya Wizara hii kupitia Programu Kuu na Programu ndogo zilizomo kama ifuatavyo: -

**Mheshimiwa Spika:** Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ina jukumu la kusimamia maeneo makuu manne ya kiutekelezaji kupitia mafungu matano ya bajeti ambayo ni fungu B01 (Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais), fungu B04 (Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira), fungu C04 (Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya) na fungu C05 (Tume ya UKIMWI).

**Mheshimiwa Spika:** katika **fungu B01** – Fungu la Afisi wa Makamu wa Kwanza wa Rais Afisi kuu - Pemba. Kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, imetengewa kiasi cha Shilingi 832,963,436 hadi kufikia mwezi Machi,

2025 imepatiwa kiasi cha Shilingi 616,441,477 (shilingi 409,116,244 kwa ajili ya mishahara na shilingi 206,225,333 kwa matumizi mengineyo) sawa na asilimia 74 ya utekelezaji wa programu.

**Mheshimiwa Spika:** kupitia Programu Ndogo (SB010303) ya Uratibu na Utekelezaji wa shughuli za OMKR Pemba yenye lengo la Kuimarisha mazingira ya kufanyia kazi na utoaji wa huduma kwa upande wa Uratibu wa Shughuli za Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mwaka 2024/2025 imefanya ukarabati mkubwa wa Nyumba ya Mapumziko ya Mheshimiwa Makamu wa Kwanza wa Rais ilioko Micheweni Pemba wenye thamani ya Shilingi 497,470,915. Kamati inaipongeza Wizara kutokana na mafanikio matengenezo hayo waliyoyafanya na inasisitiza wasimamizi wa nyumba hiyo kuitunza na kuiweka katika mazingira yakuridhisha.

**Mheshimiwa Spika:** kupitia Programu kuu PB0102 ya usimamizi wa Masuala ya Watu wenye Ulemavu, kamati inaipongeza Wizara kwa kuzipatia ruzuku Jumuiya 12 za Watu wenye Ulemavu zenye thamani ya TZS. 30,000,000 Unguja na Pemba pamoja na mikopo kwa Watu wenye Ulemavu yenye thamani ya TZS. 30,000,000 (Unguja TZS. 22,000,000 na Pemba TZS. 8,000,000) kwa ajili ya kujishughulisha na kazi za uchumi na maendeleo. Fedha hizo zimetolewa kupitia Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (ZEEA) kupitia Programu ya 4:4:2 kwa vikundi saba (7).

**Mheshimiwa Spika:** Kamati imeridhishwa na utekelezaji wa shughuli za Wizara hii juu ya kusimamia masuala yanayohusu Watu wenye Ulemavu. Hata hivyo, inaishauri Wizara kuhakikisha fedha zilizotengwa kwa ajili ya kutoa mikopo kwa vikundi vya Watu wenye Ulemavu zimewafikia walengwa na zimetumika kwa malengo yalikusudiwa. Aidha, Kamati inavitaka vikundi vyote ambavyo vimeweza kupatiwa mikopo ya fedha hizo kuzirudisha kwa wakati unaofaa fedha walizopatiwa ili ziweze kuvinufaisha vikundi vyengine vyenye

dhamira ya kukopa. kipekee, Kamati inaishukuru Serikali kwa kukubali kuwapatia mikopo watu wenye ulemavu hata akiwa mmoja mmoja au wawili.

**Mheshimiwa Spika:** miongoni mwa kazi zinazosimamiwa na wizara hii ni kuhakikisha wanaendeleza uhifadhi wa mazingira na mali asilia kwa kuzingatia utekelezaji wa sheria za nchi na miongozo ya kimataifa. Kupitia **Fungu B04** la Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira, Zanzibar. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuweza kuandaa kanuni ya matumizi salama ya bioteknolojia ya kisasa na kanuni ya biashara ya kaboni ya mwaka 2024 ambazo ziko tayari kwa matumizi. Kamati inaitaka Wizara kuzitumia kwa uadilifu kanuni hizo na kuachia mbali suala la muhali pindipo ikitokea uharibifu wa mazingira. Aidha, kamati inaishauri Mamlaka kuishirikisha jamii juu ya matumizi sahihi ya biashara ya kaboni ili kukuza uchumi wao na kuisaidia Serikali kufikia malengo ya kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi. Vile vile kamati inaishauri Serikali kuweka mkazo wa kutoa elimu kwa wananchi juu ya kulinda mazingira.

**Mheshimiwa Spika:** kamati wakati ikipitia bajeti hii imepokea taarifa za kusikitisha za kuongezeka kwa mmong'onyoko wa maeneo ya fukwe na maeneo 147 yanayoingia maji ya chumvi Unguja na Pemba ambayo yanapelekea mahitaji makubwa ya rasilimali fedha katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, tunaiomba Serikali kulipa umakini mkubwa suala hili hasa kwa kutenga fedha za kutosha katika bajeti hii 2025/2026 ili iweze kuinusuru hali hii mbaya inayoendelea kujitokeza isiweze kuendelea kuleta athari kwa jamii.

**Mheshimiwa Spika:** kwa upande wa **fungu la C04** – Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kwa mwaka 2024/2025 Kamati imeridhishwa na juhudi za Mamlaka kwa kufanikiwa kukamata na kutaifisha mali zinazohusishwa na biashara haramu ya dawa za kulevya zenye thamani wa

shilingi Milioni 976,052,016 kutoka kwa wahalifu pamoja na kuteketeza vielelezo vya dawa za kulevya vyenye uzito wa Kilogramu 1,619.86 (1,448.9 - Unguja na 170.9 - Pemba). Kamati inaishukuru Serikali kwa kuridhia kufanywa kwa marekebisho kwa sheria iliyopelekea kuanzishwa kwa Mamlaka ya Udhibiti na Kupambana dhidi ya dawa za Kulevya Sheria Nambari 8 ya 2021 iliyopewa uwezo wa kukamata, kushtaki pamoja na kutaifisha mali zitokanazo na baishara haramu za dawa za kulevya ambayo mafanikio yake yanaonekana.

**Mheshimiwa Spika,** Kupitia Programu Kuu [PC0401] ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya, Kamati inaipongeza Mamlaka kwa kazi nzuri wanazozifanya juu ya kupunguza uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa dawa za kulevya nchini. Hata hivyo, Kamati inaishauri Mamlaka kuongeza kasi ya udhibiti wa uingizaji, usambazaji na utumiaji wa dawa za kulevya ambapo licha ya juhudi hizi kubwa zinazofanywa lakini bado tatizo la matumizi ya dawa za kulevya kwa jamii linazidi kuongezeka na jamii inakosa nguvu kazi kwa maendeleo ya taifa.

**Mheshimiwa Spika,** Sambamba na hayo, Kamati pia, inaitaka Serikali kupitia miradi ya maendeleo kuharakisha ujenzi wa kituo cha Tiba na Marekebisho ya Tabia Kangagani Pemba ambacho hatua za utekelezaji wa Mradi wa ujenzi huo hadi sasa upo katika hatua za awali za kwa kumtafuta mzabuni wa ujenzi ambapo jumla ya shilingi 2,550,000,000 na Tzs. 125,039,827 zilitumika sawa na asilimia 4.9 ya fedha yote iliyopangwa.

**Mheshimiwa Spika:** Kupitia **fungu la C05** (Tume ya UKIMWI). Tume hii ina jukumu la Uratibu, Ufuatiliaji na Tathmini ya Muitiko wa Taifa wa UKIMWI yenye lengo la kujenga ufanisi katika kuratibu sekta za umma kwa kuweka miundo na mikakati imara itakayoweza kusimamia muitiko wa taifa wa VVU na UKIMWI ifikapo mwaka 2030. Kamati inaitaka Tume kupitia utekelezaji wa Programu ndogo ya Uratibu, ufuatiliaji na tathmini ya muitiko wa taifa wa

UKIMWI, kuhakikisha malengo yote yaliyopangwa katika Bajeti hii yanatimia kwa ufanisi mkubwa ikiwa pamoja na kupunguza athari za maradhi yenye kuambukiza ikiwemo VVU na yasio ambukiza, ingawa kwa mujibu wa taarifa ya Tume hali ya maambukizi bado ni mbaya na inazidi kuhatarisha maisha ya jamii hususan Mikoa ya Kusini na Kaskazini Unguja ambayo maambukizi yamekuwa yakiripotiwa kwa hali ya juu.

**Mheshimiwa Spika,** Sambamba na hayo, Kamati inazidi kusisitiza kuwa Serikali iongeze fedha za maendeleo kwenye Tume ya UKIMWI Zanzibar ili kwenda sambamba na fedha zinzotolewa na wahisani wa maendeleo kwa lengo la kuiwezesha Tume kutimiza majukumu yake kwa asilimia iliyojiwekea.

**Mheshimiwa Spika,** Mwisho, nitumie fursa hii tena kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kunijaaliwa kuwasilisha maoni haya kwa utulivu wa hali ya juu. Pia, napenda kukushukuru tena kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni ya Kamati yangu kwa niaba ya Kamati pamoja na kuwashukuru Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa umakini mkubwa. Sasa niwaombe Wajumbe wa Baraza lako tukufu waijadili na hatimae waiunge mkono bajeti hii ili wamuwezeshe Mheshimiwa Waziri kufanikisha na kutekeleza yale waliojipangia katika mwaka mpya wa Fedha 2025/2026.

**Mheshimiwa Spika,**
Kwa niaba ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa naunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha.

***Ahsante;***

……………………………

***(Machano Othman Said)***

Mwenyekiti,

Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa,

**BARAZA LA WAWAKILISHI,**

**ZANZIBAR**